TANGAZO LA SERIKALI NA. 416 la tarehe 23/6/2023

SHERIA YA TOZO ZA BARABARA NA MAFUTA,
(SURA YA 220)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8)*

AMRI YA MSAMAHA WA TOZO YA BARABARA NA MAFUTA KWA MRADI WA KUHIFADHI NA KUENDELEZA MFUMO WA IKOLOJIA WA SELOUS (SECAD) (WIZARA YA MALIASILI NA UTALII) YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Tozo ya Barabara na Mafuta kwa Mradi wa Kuhifadhi na Kuendeleza Mfumo wa Ikolojia wa Selous (SECAD) (Wizara ya Maliasili na Utalii) ya Mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tarehe 23 Mei, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, tozo zote za barabara na mafuta kwa mafuta yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii yaliyoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Wizara ya Maliasili na Utalii au kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya Mradi wa Kuhifadhi na Kuendeleza Mfumo wa Ikolojia wa Selous (SECAD) zinasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na tozo za barabara na mafuta zitapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa mafuta yatatumika kwa matumizi mengine au yatahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafikia ukomo tarehe 30 Juni, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| NA. | Maelezo | Kipimo | kiwango |
|---|---|---|---|
| 1. | Dizeli | Lita | 1,900,000 |
| 2. | Petroli | Lita | 2,300 |

Dodoma,
10 Juni, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha na Mipango*